

HABARI KITAIFA/TANGAZO

KERO

Adha kukosekana usafiri wa mwendokasi Dar

Na Beatrice Moses

KUTOKANA na uharibifu wa miundombinu ya usafiri wa mwendokasi jijini Dar es Salaam, uliosababishwa na vurugu wakati wa Uchaguzi Mkuu, Oktoba 29 serikali iliamua kusitisha usafiri huo ambao sasa umegeuka kuwa kero kwa wananchi wanaotegemea usafiri wa umma, wakilazimika kutumia mbadala wa bajaji na pikipiki unaogharimu zaidi ya kipato chao cha kila siku.

Kusitishwa kwa huduma hiyo ni kuruhusu kufanyika kwa tathmini ili kujua uharibifu uliofanyika.

Vurugu hizo zilisababishwa na waandamaji ambao waliharibu miundombinu ikiwamo ya vituo vya mwendokasi, kuvunja na kuvichoma moto na kuharibu mifumo ya ukataji wa tiketi, pamoja na kutetekeza baadhi ya mabasi.

Kwa mujibu wa wananchi waliongea na Nipashe, madhara ya uharibifu huo yamekuwa usumbufu mkubwa kwao kwa kusababisha gharama za usafiri kuongezeka na mabasi yaliyochukua nafasi ya kutoka huduma hiyo kutotosheleza mahitaji.

Clementina Fredrick, mkazi wa Kibanda cha Mkaa, eneo la Mbezi, jijini Dar es Salaam alisema tangu kusitishwa kwa huduma hiyo, hakuna tena uhakika wa usafiri kwa kuwa daladala zinazopita eneo hilo zinakuwa zimeshajaa.

"Shughuli zangu zipo Kariakoo, hivyo nipanda bajaji hulazimika kulipa kati ya Sh. 3,000 hadi 5,000, kutegemea na hali ya usafiri siku hiyo. Wakati mwingine hulazimika kuvuka upande wa pili nipande daladala la



Abiria wakiwa wamelundikana wakisubiri usafiri wa daladala katika kituo cha Kimara Mwisho, Dar es Salaam jana, kutokana na kukosekana kwa usafiri wa mwendokasi uliositishwa na serikali. Picha: IMANI NATHANIEL

Mbezi, lakini foleni huwa kikwazo kikubwa," alisema Clementina.

Amesema usafiri wa mwendokasi ulikuwa na nafuu zaidi kwa kuwa foleni zilidhibitiwa na wakati mwingine wasimamizi walihakikisha magari tupu yanaanzia katika vituo vya kati, hali iliyosaidia abiria kufika kwa wakati.

Clementina Fredrick, mkazi wa Kibanda cha Mkaa, eneo la Mbezi, jijini Dar es Salaam alisema tangu kusitishwa kwa huduma hiyo, hakuna tena uhakika wa usafiri kwa kuwa daladala zinazopita eneo hilo zinakuwa zimeshajaa.

Zebedayo Mika, mkazi wa Temboni, amesema analazimika kutumia usafiri wa pikipiki kwa mtindo wa mshikaki ili kuhakikisha anawahi kazi kwake.

"Najua siyo salama kwangu, lakini nalazimika kutumia pikipiki kwa kuwa nina uhakika wa kufika ofisini kwa wakati. Naweza kulipa kati ya shilingi 3,000 hadi 4,000 kutoka hapa hadi Mnazi Mmoja," alisema Mika.

Amina Kingu, mkazi wa Goba, alisema sasa analazimika kuamka saa 10 alfajiri pamoja na wanawe wanaosoma mjini ili kufika kituo cha Mbezi kutafuta usafiri.

"Tulipokuwa tunatumia mwendokasi kulikuwa na utaratibu mzuri wa kupanda magari kwa foleni, wanafunzi waliheshimika na huduma ilikuwa nafuu. Sasa foleni ni kero na tishio kwa ajira zetu," alisema Amina.

Katibu wa safari za daladala za Mbezi - Mwananyamala, Sammata Shaban, amesema hivi sasa kuna magari 47 yanayofanya safari hizo baada ya kupokewa magari mawili mapya kutoka 45 za awali.

Nurdin Awadhi, Msaidizi wa safari za Goba - Kawe na Goba - Makumbusho, amesema abiria wanakumbwa na usumbufu mkubwa kutokana na uhaba wa magari yanayokwenda Mnazi Mmoja.

"Abiria wanagombania magari kwa kuwa ni machache. Mabasi ya mwen-

dokasi yalikuwa makubwa, haya ya sas ni coaster zenye uwezo wa kubeba abiri 25 tu. Asubuhi ndiyo usumbufu mkubwa zaidi," amesema Awadhi.

Jackson Mwilambo, Mwenyekiti wa usimamizi wa safari za daladala za Mbezi - Muhimbili, amesema ni magari 10 pekee yanayofanya safari hizo kwa sasa wakati uhitaji ni mkubwa.

"Kwenye mwendokasi walikuwa warapanda kwa foleni, lakini sasa ni kupambana kupata kiti, gari ni chache na abiri ni wengi, jambo hili ni hatari, hivyo suhesho linahitajika haraka," alisem Mwilambo.

Aidha, Aloyce Mfoi, dereva wa basaina ya Hecher linalofanya safari ya Mbezi - Mnazi Mmoja, amesema gharama za kuchora maandishi ya safari zimekuwachangamoto kwa wamiliki wa magari.

"Imeniharimu Sh. 125,000 kulipakmkanda na kuchora maandishi ya safar jambo ambalo linaongeza mzigo kwa wamiliki," alisema Mfoi.

Hata hivyo, Mamlaka ya Udhidhizi Usafiri Ardhi (LATRA) ilitoa tangazo Novemba 5, mwaka huu ikieleza kuwa, katik juhudi za kurejesha huduma za usafiri wa abiria kwenye Barabara ya Morogoro na njia ya Mabasi Yaendayo Haraka (BR-1), imetoa vibali vya muda kwa mabas ya kawaida kufanya safari kadhaa.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, safari zilizotolewa vibali ni pamoja na: Mbezi Luis - Makumbusho kupitia Morogoro Kawawa, Mwananyamala (daladala 25), Mbezi Luis - Mnazi Mmoja (daladala 50), Mbezi Luis - Muhimbili (daladala 25) n Mbezi Luis - Posta kupitia Morogoro, Bit Titi, Maktaba.

Vibali hivyo ni vya muda wa miezi mitatu na vitahitishwa kulingana na hali ya huduma za BRT hadi sasa zimepatikana.

Afisa Leseni Mwandamizi wa LATRA Patel Ngereza, alisema uamuzi wa kutoa vibali hivyo vya muda unalenga kuhakikisha wananchi hawakosi hudum muhimu ya usafiri wakati jitihada za kurekebisha mfumo wa mwendokasi zikiendelea.

"Bado tunaendelea kutoa wito kwa wamiliki wa magari kujitokeza kusajili ilikupata vibali vya kutoa huduma hii. Nafursa nzuri na muhimu kwa wananchi, alisema Ngereza.

TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA MWISHO WA WANAHISA WA KAMPUNI YA

PRICEWATERHOUSECOOPERS SERVICES LIMITED

Cheti cha Usajili No. 34477

Sheria ya Makampuni[Sura ya 212 Toleo la :2023] (Kifungu 348 (1))

Umma na wahusika wanafahamishwa kutakua na mkutano mkuu wa mwisho wa wanahisa wa kampuni la Pricewaterhousecoopers Services Limited, yenye usajili namba 34477 kitakachofanyika tarehe 15 Desemba 2025 ofisini kwa mfilisi saa 4:00 asubuhi ambapo mfilisi atatoa hesabu ya kufungwa kwa hiari kwa kampuni.

Mfilisi **JOSEPH LYIMO**Amwani ya Mfilisi **PricewaterhouseCoopers Limited, Pemba House, 369 Toure Drive, Oyster Bay. P.O. Box 45. Dar es Salaam. Tanzania**Tarehe ya kuchaguliwa **18 JANUARY 2023**Amechaguliwa na **WAMILIKI WA KAMPUNI**

Sahihi

Tarehe: 13/11/2025

Jina: **JOSEPH LYIMO**

Imetolewa na;

JOSEPH LYIMO**PRICEWATERHOUSECOOPERS SERVICES LIMITED**

The Citizen Friday November 14, 2025 Pg 2

New era as Latra promotes smart, sustainable mobility

By Hellen Nachilongo
@musanachi60
hnachilongo@tz.nationmedia.com

Dar es Salaam. Bus manufacturers and vehicle assembly firms are preparing to showcase new innovations aimed at transforming Tanzania's public transport sector.

Land Transport Regulatory Authority (Latra) Director General Habibu Suluo said the first-ever Sustainable Land Transport Week will also feature international industry players, including Yutong and HOWO, demonstrating energy-efficient vehicles and smart fleet-management solutions tai-

lored for the African market. The event is scheduled for November 24-29 and will follow the Latra Awards for outstanding service providers.

"Over 800 participants from across the globe will engage in discussions on sustainability, innovation, safety, customer care and operational efficiency in the land transport industry," said Mr Suluo at a press briefing yesterday.

He added that the event will offer daladala, truck and bus owners the opportunity to interact directly with manufacturers and assembly companies, particularly to explore the purchase of electric vehicles.

The awards recognise outstanding and responsible operators

MR SULUO | LATRA

Speaking on the awards, Mr Suluo noted that under Section 6, Act, Cap 413, Latra is mandated to foster effective competition among regu-

lated service providers.

"The awards recognise outstanding and responsible operators, improving competition and strengthening the transport ecosystem," he said.

Mr Suluo also highlighted improvements in service quality, noting that operators have invested in luxury buses and enhanced customer experience.

"Despite challenges, we have not seen strikes or major disruptions because operators continuously seek innovative solutions," he said.

The awards will recognise inter-city passenger bus operators, cargo transporters, ride-hailing services,

providers of vehicle-tracking technologies and journalists or media outlets promoting road safety and quality service.

Latra has also begun certifying truck drivers and passenger service operators to ensure professionalism and accountability.

"The awards are not merely ceremonial. They drive sustained reliability, innovation and efficiency," Mr Suluo said.

"As a country, we cannot progress in isolation. Collaboration with stakeholders, particularly in sectors like agriculture where transport is vital, contributes to national economic growth," he said.